R5166

# KIFO NA UFUFUO

KIFO SI kulala;ni Uharibifu.Miili iliyokufa inaoza kwa sababu ya kazi ya uharibifu inaendelea kwayo.Twasema kwamba aibu inaingia;yaani uharibifu wa tishu inaendelea hadi kila kitu kilichokuwa na uhai katika mwili huo kinapotea.Mchakato huu wa kuoza ni sawa kwa binadamu na kwa mnyama,na pia hata kwa ulimwengu wa mboga.Kama vile Maandiko yanavyosema, "kwa maana linalowatukia wanadamu linawatukia wanyama;jambo moja linawatukia;anavyokufa huyu ndivyo anavyokufa huyu;naam,wote wanao pumzi moja;wala mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyama….Wote huendea mahali pamoja;wote hutoka katika mavumbi;na hata mavumbini hurudi tena."-*Mhubiri 3:19,20.*

Watu wengi wanaonekana kuchanganyikiwa kuhusu maana ya  neno " nafsi." Mafundisho ya kimaandiko ni kwamba mwanadamu ni nafsi.Katika *Mwanzo 2:7* twasoma, " BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi,akampulizia puani pumzi ya uhai;mtu akawa NAFSI HAI." Neno la Mungu linatambua mwanadamu na mnyama kama nafsi. (Tazama *Hes.31:28*).Mwili,nafsi na roho zote kwa pamoja zinapatikana katika kiumbe hai.

Mbwa ana mwili;mbwa ana uhai-kanuni muhimu sana;na tofauti na kanuni ya uhai na kiumbe,mbwa ana utu.Mbwa mmoja anatofauatiana na mwingine;mmoja anaweza kuwa mkali,mwingine awe mpole kwa familia ya waastarabu.Kila mnyama ana njia yake ya furaha na huzuni;lakini kwa vyovyote vile,vitu hivi vyote vinatengeneza uzoefu kwa mbwa kupata kujitambua mwenyewe.

Basi hivyo ndivyo ilivyo kwa mwanadamu.Kuna mwili na kanuni ya uhai,muungano ambao unaunda nafsi.Uzoefu wake-maisha yake ya nyumbani,elimu yake,mazingira yake,usafiri wake,pesa zake,masuala yake nyeti-yote yanaunda utu wake.Sio mwili wake,lakini ni nafsi yake ndiyo ina uzoefu huo.Kama vile mbwa wawili walio katika uzoefu tofauti wanakuwa na utu tofauti,basi hata na wanadamu pia.Uzoefu wote tofauti wa maisha unasaidia kuunda furaha au huzuni,waliojifunza au wasiojali,wenye hakima au wapumpavu.

## KATIKA MAUTI MWANADAMU ANA UMUHIMU GANI?

Tofauti gani iliyoko kati ya nafsi ya hayawani na ya binadamu? Nafsi ya mwanadamu ina mpangilio wa mwili na ubongo ulio wa juu,ambao unamfanya mwenye mpango wa juu;lakini sio kwamba amepewa ubongo bora kwa njia ile tukufu,lakini hakuumbwa kama hayawani wasio na akili ili afe kwa muda wa miaka michache.Binadamu aliumbwa ili apate kuishi milele.

Katika Edeni,binadamu alifikia hukumu ya kifo,kama adhabu ya uasi.Wazao wote wamezaliwa chini ya masharti ya kifo.Kila mwanadamu anapokea cheche ya uhai kutoka kwa wazazi wake,la sivyo mwili ungerudi mavumbini.Wakati mtu amekufa,utu wake,ambao unarithiwa na ushawishi kabla hajazaliwa ukiungana na uzoefu wake,unapotea;kwa sababu haziwezi kuishi bila

mwili.Kama vile Maandiko yanavyotangaza, “ Katika siku hiyo MAWAZO yake *hupotea*,” wafu hawajui *neno lo lote*,”; “kwa kuwa hakuna kazi,wala shauri,wala maarifa,wala hekima,huko kuzimu uendako wewe.”-*Zab.146:4;Mhub.9:5,10*.

Swali basi latokea,Je! Mwanadamu pia anakufa kama vile uumbaji wa hayawani wanavyokufa? Twajibu hilo swali kwamba mwanadamu anakufa kama mnyama,ikiwa Mungu hangepanga maisha ya baadaye ya mwanadamu.Mungu anapanga kurejesha uhai,sio mwili,lakini nafsi iliyokufa.Nafsi iliyokufa ndiyo nafsi iliyokombolewa na Yesu.-*Zab.49:15*.

Kupitia kwa ufufuo,Mungu amepanga kuonyesha upendo wake kwa ulimwengu.Imeandikwa, “Hata ulipowadia utimilifu wa wakati,Mungu alimtuma Mwanawe” (*Wagalatia 4:4*); “ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote” (***1 Timotheo 2:6***)- “kwa kila mtu.” (*Waeb.2:9*)..Kila mtu ameenda kwa kifo ama anaelekea huko;kama ukombozi haungetolewa,basi hatungekuwa na ufufuo.Basi Mtume Paulo anaeleza jambo hilo kwamba, “ Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu,kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu.Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa,kadhalika na katika Kristo wote wanahuishwa.Lakini kila mmoja mahali pake;limbuko ni Kristo;baadaye walio wake Kristo,atakapokuja.”-*1 Wakorintho 15:21-23*.

Kuhuisha basi ndiyo ufufuo wa wafu-sio chembe cha mata ambayo imetengeneza mbolea kwa miti na kupitia kwa matunda yake imetengeneza kiumbe kingine,lakini ni ufufuo wa mtu-nafsi.Katika ufufuo, “ lakini Mungu huipa mwili kama apendavyo,na kila mbegu mwili wake.” ( ***1 Wakorintho 15:38***).Kwa mtu binafsi,haijalishi ni chembe gani kinatengeneza mwili mpya.Kile ambacho anataka ni ufufuo wa nafsi-roho yake-utu wake.Ule urejesho ndio sehemu muhimu sana katika ufufuo.

Mungu ametoa hakikisho kwamba ana uwezo wa kurejesha binadamu;na sisi ambao tumeamini Neno lake hatuchukui binadamu kwamba amekufa kama hayawani.Kwa kinyume,tunaruhusu mnyama apitie uharibifu,lakini tunafikiria juu ya binadamu.Kwa sababu kwa wafu wetu tunasimamisha ukumbusho,wa mwili ambao unawakilisha utu ulio bora kwetu.Imani yetu inatuhakikishia kwamba utu haupotei,lakini kwamba utakuwa na ufufuo.Heshima tunayoonyesha marafiki na wapendwa wetu wakiwa makaburini inaonyesha Imani yetu katika uhai wao wa siku za usoni kupitia kwa ufufuo wa wafu.

## KIFO CHA KIADAMU KIMAANDIKO KINAITWA USINGIZI

Katika Maandiko,Mungu anazua wazo kwamba wafu wanalala usingizi.Kwa vile yeye ndiye ana Nguvu na Kusudi la kufufua mfu,anaweza kuongea kuwahusu kwa njia hiyo.Miili yao kwa hakika imeenda mavumbini,lakini wao kama binafsi Mungu anawajua.Kufufua watu kutoka mautini na kuwapa mawazo waliokuwa nayo kabla hawajafa itakuwa kazi ya ajabu,ambayo Hekima na Nguvu ya Mwenyezi Mungu ndizo zinaweza kukamilisha.Wale tu wanao ujasiri katika ahadi za Mungu ndio wanaweza kujua kuwa wapendwa wao kama waliolala katika mauti.

Maandiko yanaongea kwa wenye Imani waliokufa kama waliolala.Twasoma kwamba “Daudi alilala na baba zake.” ( ***1 Wafalme 2:10***).Maelezo hayo pia yametolewa kuhusu wafalme wote wa Israeli,wema na wabaya.Mtakatifu Stefano,aliyepigwa mawe hadi akafa, “ alilala usingizi,” (

*Matendo 7:60*) Mtume Paulo alisema, " Hao waliolala katika Yesu,Mungu atawaleta pamoja naye….kwamba sisi tulio hai,tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana,hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti…nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza."-***1 Wathesalonike 4:14-16***.

Asubuhi ya Siku ya utukufu ambayo Jua la Haki atatokea na uponyaji katika mwali wake,kila kitu ambacho Mungu ameahidi kwa wakati huo utatendeka.(***Mal.4:2).***Kwa wakati huu,wafu wanangojea Siku hiyo ambapo "wote waliomo makaburini watasikia sauti yake [sauti ya Mwana wa Adamu] nao watatoka." (***Yohana 5:28,29***).Katika hali ya neno hili,basi twasema wafu wamelala.Bwana wetu alitumia neno hili akiongea kuhusu Lazaro.Alisema, " Lazaro amelala." Kwa majibu ya wanafunzi,walionyesha kwamba hawakumwelewa,Yesu akawaambia waziwazi, "Lazaro amekufa."-***Yohana 11:11-14.***

AWAMU YA KIBINGU YA UFUFUO

Kwa hali moja,watu wote wanalala ili wangoje pambazuko la Siku ya miaka elfu,wakati Jua la Haki linatokea.Ufufuo utawajia watu wote;lakini watu wawili walikuwa kwa kiwango kimoja cha uharibifu,wengine watatoka haraka kuliko wengine.Maandiko yanaonyesha kwamba kutakuwa na viwango vingi vya ufufuo.Mmoja kati yao umeitwa " Ufufuo wa kwanza," yaani,ule mkuu na wa muhimu;na utahusiana na wale watakaohusika na Bwana wetu katika Kiti cha Enzi. " Heri,na mtakatifu,ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza;juu ya hao mauti ya pili haina nguvu;bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo,nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu."-***Ufu.20:6.***

Maelezo haya hayaelezi kuhusu umati mkubwa bali yanaeleza kuhusu Kundi Dogo, "washirika wa tabia ya uungu." ( ***2 Petro 1:4***).Maandiko mengine yanatuonyesha kwamba Umati Mkubwa watapata utimilifu wa kiroho wakati wa ufufuo wao;basi twaweza kudhani kwamba yao ni ufufuo wa pili-wa pili kwa mpango,katika utukufu na katika upendeleo.Makundi yao mawili yana " Kanisa ya Wazaliwa wa kwanza,ambao wameandikwa Mbinguni." ( ***Waeb.12:23***).Tofauti kati yao tu ni kwamba Kundi Dogo walikuwa na jitihada ya kuenda mbele na kufanya majukumu yao na nafasi waliyokuwa nayo,wakati Umati Mkubwa hawakuwa na bidii na kuwa na mioyo ya kujitoa ijapokuwa walipitia kifo kuliko kumkataa Bwana na Ukweli.

Tofauti umewekwa katika mpangilio wa kawaida wa Agano la Sheria.Kama vile kabila ya Lawi waliitwa miongoni mwa Israeli kufanya kazi ya kipekee,hivyo Kanisa la Wazaliwa wa kwanza wameitwa miongoni mwa wanadamu,kama asili ya Walawi.Kabila ya kuhani ya Walawi iligawanywa katika makundi mawili,makuhani na Walawi,na pia Kanisa lina makundi mawili.Kwa makundi haya, "wanaoshinda" pekee (***Warumi 8:37***) ndio watapata kuwa "washiriki wa tabia ya uungu" na kuwa wa kwanza.Umati mkubwa hawatafikia utukufu huu.

Hatuwezi kutofautisha "wale walioshinda." Umati Mkubwa wanatambulika na Kundi Dogo hapa duniani na Mbinguni pia.Makundi haya yote ni ya " Wazaliwa wa kwanza." Kama vile Mitume Paulo anavyosema, sisi ni "limbuko la kwanza la viumbe." (***Yakobo 1:18***).Kwa kueleza wazo hili,wacha tuangalie kitanda cha matunda.Matunda haya ni miongoni ya malimbuko ya kwanza

ya misimu,japo hata miongoni mwao tunapata mengine yanaiva haraka kuliko mimea mingine.Matunda ambayo yanaiva mapema haya yanaweza kusemekana kwamba ni limbuko la kwanza ama malimbuko ya kwanza.Na hivyo ndivyo ilivyo na Kundi Dogo.

## AWAMU YA KIDUNIA YA UFUFUO

Katika Maandiko,kundi la tatu la watumishi wa Mungu wametajwa.Wengi wao wameitwa kwa majina yao katika barua kwa Waebrania.Twarejelea Waliohitimu wa Kale,ambao waliishi na kupatikana kuwa waaminifu kabla ya kuja kwa Mwokozi.Hawa hawakupata nafasi ya kufuata nyayo za Bwana na hawakuwa na "mwito mkuu." Hawa wanasemekana kupokea "ufufuo ulio bora" kuliko wanadamu wengine ( ***Waeb.11:35***)-bora,sio kwamba wamekuwa kwa ndege moja,lakini ni kwamba watapata kuhuishwa kwa utimilifu wa mwanadamu,wakati wanadamu wengine watakuwa miaka elfu wakati watakuja polepole kwa hali ya awali iliyoptezwa na Adamu.

Mwanzoni mwa utawala wa Kristo,Waliostahili wa Awali watatokea wakiwa wanadamu kamilifu-kiakili na kimwili-ili miili yao iambate na maendeleo ya kimaadili yao.Ikiwa walikuwa na jeraha,hawatakuwa nazo tena;ikiwa walikuwa na dosari,zitapotea.Siyo rahisi kwetu kuwa na taswira ya mtu mkamilifu,kwa sababu hatujawahi kumwona mmoja,na wale waliotuzunguka wana viwango vya udhaifu.Lakini twajua kwamba mtu mkamilifu atakuwa mkamilifu katika muundo,hulka,sauti,mtazamo,usikivu,ladha,na pia kwa viungo vingine vyote,na pia hata kwa mawazo.

Mwishowe, "mabaki ya watu" watafufuka, "kila mmoja mahali pake." ( ***1 Wakorintho 15:23***).Kuamka kwao kutawaleta kutoka katika hali ambayo waliingia kwa kaburi, "hakuna kazi,wala shauri,wala maarifa wala hekima." (***Mhubiri 9:10***).Huu uamsho sio ufufuo,lakini ni hatua tu ya kwanza ya ufufuo.Neno la Kiyunani la "ufufuo" ni *anastasis*,na linaamanisha "*kusimama tena*." Adamu alianguka,na tangia wakati huo "dunia yote hukaa ndani ya uovu"-kawaida lina maana kwamba "*dunia inakaa ndani ya mwovu*." ( ***1 Yohana 5:19***).Kuamka tena,basi ni kurejesha ukamilifu uliopotea pale Edeni;kwa sababu ulimwengu wa wanadamu ufufuo ni kufanywa upya.-***Matendo 3:19-21.***

Wakati wa utawala wa Masihi wa miaka elfu ,ufufuo wa ulimwengu utaendelea.Kazi haitafanywa na Baba mwenyewe,lakini atakabidhi hiyo kazi kwa Bwana Yesu (***Yohana 5:28,29***),na itachukuwa muda wa miaka elfu mizima ili ipate kukamilika.Mwishoni mwa utawala wa miaka elfu wa ulimwengu wa wanadamu watakuwa wakamilifu,kama vile Adamu alivyokuwa wakati wa uumbaji.Kazi zote za Mungu ni timilifu.-***Kumb.32:4;Mwanzo.1:31***.

Kama vile imeelezwa,Watakatifu wa Kale,watapewa ufufuo bora kuliko watu wengine kama ujira kwa Imani yao kwa Mungu.Wengine waliobaki watafufuka katika hali ile waliokuwa nayo wakati walikufa.Hawatajua jambo jingine zaidi au kupungukiwa jambo zaidi ya yale waliyokuwa wakiyajua kabla hawajafa,utu wao utakuwa sawa vile ilivyokuwa.Kuhusu miili yao,hatuwezi kusema kwamba itakuwa kamilifu,kwa sababu ikiwa wanadamu wangefufuliwa kutoka kwa mauti,hawangejua wengine.Ikiwa wote wangehuishwa wakiwa na rangi moja,ama ikiwa wote

wangeletwa na mtindo mmoja wa tabia,hawangetambulika.Basi watahuishwa sio kwa njia ya kushindwa kupumua,ama kwa vipande vipande,kana kwamba walipulizwa na upepo ama kana kwamba waliliwa na mnyama,lakini kwa ile hali yao ya afya.

Wanadamu wanapata kujitambua kwa sifa nyingine za kawaida na pia tabia ya akili na maadili.Ikiwa katika kuhuishwa atapewa ubongo mkamilifu,hatajijua wakati anatoka kwa kaburi.Mawazo yake yatakuwa tofauti;hakuna kitu ambacho kitawafanya wajitambue.Wanadamu watahuishwa kutoka kaburini katika hali iliyopendekezwa na Bwana wetu wakati alimwambia mtu aliyepoozwa mkono, “Nyosha  mkono wako!” Naye akaunyosha;mkono wake ukawa mzima tena” ( ***Luka 6:10***)-kwa ukamilifu-siyo kwa hali yote timilifu,lakini ile inayotosha kuanza uhai upya.

## AIBU NA KUDHARAULIWA ZITATUPWA MBALI WAKATI WA MILENIA

Mwokozi alifanya upatanisho kwa dhambi ya wanadamu kwa kusudi la kuwapa jaribio la uhai,nafasi ya kuonyesha ikiwa katika Ufalme wa Masihi,kwa hali inayofaa,watachagua haki na uhai ama maovu na mauti ya milele.Maandiko yanaonyesha kwamba kutakuwa na aibu kubwa na madharau ambayo yatashika wale ambao hawatakuwa katika mkataba na Mungu.-***Dan.12:2***.

Wakati wa miaka elfu wa majaribu,wengi watatupa aibu na madharau.Kwa hiyo twaweza kusema kwamba ,miaka ikizidi kusonga,aibu itapita polepole na madharau yatapotea kabisa.Twaona hoja hii ikielezwa kuhusu hali ya Sauli wa Tarso.Wakati aligundua kwamba alikuwa akienda dhidi ya Mungu,aliaibika sana kwa kile alichokuwa akitekeleza.Pole pole alianza kuonyesha uaminifu wake kwa Mungu,alijiondoa aibu yake na madharau.Ujasiri na juhudi katika huduma ya Bwana ziliondoa vitu alivyofanya pasipojua Saulo wa Tarso.Aibu yake ,basi ilipotea.

Ulimwengu utaamka kutoka kwa wafu katika hali hii ya aibu na madharau.Lakini polepole watiifu watazidi kuendelea kwa hali ya awali ya ukamilifu wa sura ya Mungu.Na wale wasiotii kabisa kwa kujua,kwa upande mwingine,hawataendelea.Watazama chini,hadi mwishowe wataingia katika uharibifu wa milele,ama kama vile Mtakatifu Petro anavyosema, “Lakini hao kama wanyama wa  wasio na akili…wataangamizwa katika maangamizo yao.” -***2 Pet.2:12***.

Wakati alipokuja mara ya kwanza Bwana wetu alifanya uponya mara nyingi siku ya Sabato,basi hii inaonyesha kazi ya uponyaji atakaofanya kwa ulimwengu siku kuu ya Sabato ya asili-Miaka elfu.Wanadamu watatokea kaburini wakiwa huru kutoka kwa dhuluma ya awali,na miili ya wanadamu katika hali nzuri,ili kwamba marafiki zao wapate kuwatambua kama walivyokuwa wakiwatambua awali;lakini watakuwa na udhaifu-ya kimwili,kiakili na kimaadili.

Mungu ametoa kila kitu kinachotakikana kwa ufufuo wa wanadamu-siyo gharama ya Fidia pekee,lakini pia Ufalme wa upatanisho wa Kristo.Ushawishi mkubwa wa Awamu unaokuja utafunguliwa kwa kila mshiriki wa jamii,wakiwa wakuu au wadogo,wenye mali au maskini.Lakini kukubali kwao au kukataa kwao  na jinsi watakavyozidi kuendelea kutategemea mvuto wao wa kibinafsi katika swala.Wale ambao wamekataa kuendelea na kukosa kuonyesha hamu ya kuendelea,watakatizwa katika Mauti ya Pili.

Hakuna sababu ambayo itafanya wasiotaka kuendelea kuruhusiwa kuishi milele.Haki ile ambayo inatangaza kwamba wale tu ambao wamekuwa katika umoja mkamilifu na Mungu watakuwa na uzima wa milele,haitaruhusu hao wasiokamilifu kuendelea kuwa wabaya.Hiyo itaonyesha kwa tabia yao kwamba hawajakuwa katika amani na haki,na kwa hivyo watakuwa kwa kundi la waovu.Kuhusu hawa,imeandikwa, “ Na wote wasio haki atawaangamiza.” –***Zab.145:20***.

====================